# Ulinganishaji wa Maumbo na Miundo ya Ukanushi katika Lugha ya Kiswahili naKiingereza

*Issaya Lupogo**

**Ikisiri**

*Kiingereza ni moja kati ya lugha ambazo wataalamu wengi wameandikia kuhusu ukanushi tofauti na Kiswahili ambacho ukanushi umechunguzwa na wataalamu wachache. Hali hii inawalazimu wanaisimu wanaoandika kuhusuukanushi katika Kiswahili kusoma kwanza mijadala ya ukanushi katika lugha ya Kiingereza kwa sababu ndiyo machapisho yaliyopo kwa wingi katika taasisi za elimu ya juu nchini Tanzania.Kutokana na hali hiyo, ni kawaida kuona uchambuzi wa ukanushi katika lugha ya Kiswahili ukiathiriwa na misingi ya uchambuzi wa ukanushi wa lugha ya Kiingereza.Ili kuondokana na hali hii katika Kiswahili, inafaa kuchunguza mfanano na tofauti za maumbo ya ukanushi baina ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Jambo hili litawasaidia wanaisimu watakaomakinikia suala la ukanushi katika Kiswahili kutoathirika sana na misingi ya uchambuzi wa ukanushi wa lugha ya Kiingereza.Makala hii ni matokeo ya utafiti wa maktabani ambapo mwandishi amepitia maandiko mbalimbali kuhusu ukanushi katika Kiingereza na maandiko ya sarufi ya Kiswahili ambayo ndani yake kuna vipengele vya ukanushi pamoja na makala moja inayohusu mofosintaksia ya ukanushi katika Kiswahili. Data hizo zimepanuliwa na mwandishi[1] ambaye ana tajiriba ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Makala imebaini kwamba kuna maumbo na miundo ya ukanushi katika lugha ya Kiingereza ambayo inakaribia kuendana na ile ya lugha ya Kiswahili. Pia, kuna maumbo na miundo inayotofautiana kabisa baina ya lugha hizi mbili. Vilevile, kuna ufafanuzi wa masuala machache ya ukanushi katika Kiswahili ambayo hayakumakinikiwa na wanaisimu waliotangulia.*

**Key words:** *Kiingereza, Kiswahili, ukanushi, mofosintaksia, uchambuzi, maumbo, miundo*

**Abstract**

*English is one of the languages in which negation has intensively been discussed compared to Kiswahili where this category has been discussed by just a few scholars. This situation forces scholars who want to write about negation in Kiswahili to review negation in English as part of their literature review. This is due to the fact that the libraries in Tanzanian higher learning institutions are full of English based language literature presumably because a lot of research involved English while research in languages like Kiswahili is still infant. That being the case, it is obvious that analysis of negation in the Kiswahili language is always affected by English negation analysis principles.*

* Assistant Lecturer, Department of Languages and Communication Studies, Mzumbe University, P.O. Box 5, Mzumbe, Morogoro, Tanzania, E-mail: *islupogo@mzumbe.ac.tz*

*Therefore, it is important to investigate the similarities and differences of negators between Kiswahili and English. This will help scholars working on negation in Kiswahili not to overrely on the negation analysis principles based on the English language. This is a literature-based paper in which the author reviews several sources about English negation in English. Kiswahili grammar books & dissertations which consist of some parts of negation matters are also reviewed. One paper which addresses the morphosyntax of negation in Kiswahili is also discussed. These data from the surveyed literatureis backed up with the author's[2] data based on him as a competent Kiswahili speaker and a seasoned language teacher. The paper shows that some negators in English behave like those in the Kiswahili language. In the paper, there are other negators which are totally different in these two languages, showing that each is a language in its own right. The paper also highlights some Kiswahili negation matters which have not yet been captured by previous scholars and thereby sparking a new debate on negation.*

## Utangulizi

Ukanushi ni mchakato wa kisarufi uoneshao upingaji wa maana ya sentensi (Crystal, 1993). Hii ni sawa na kusema kwamba ukanushi ni kinyume cha hali ya uyakinishi. Ukanushi ni suala lililopo katika lugha zote za ulimwengu (Lindstad, 2007).

Kiswahili ni moja ya lugha za Kibantu zinazozungumzwa barani Afrika na nchi nyingine kadhaa ulimwenguni. Kiswahili sanifukimetokana na kusanifishwa kwa lahaja ya Kiunguja baada ya lahaja iliyokuwa ikikaribiana nayo kiushindani, Kimvita kuachwa. Katika kipindi cha ukoloni, paliibuka mjadala miongoni mwa watawala kuhusu lugha ipi itumike ukanda wa Afrika Mashariki (Kenya, Uganda, na Tanganyika) katika sekta zote rasmi. Ndipo Kiunguja (baadaye Kiswahili sanifu) kikachaguliwa miongoni mwa lugha nyingi zilizokuwapo na baadaye lugha hiyo ilisanifishwa. Mchakato wa kusanifisha Kiswahili ulianza mwaka 1930 ambapo serikali ya kikoloni iliunda Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki (kwa sasa ni Taasisi ya Taaluma za Kiswahili - TATAKI[3] ) na kuiagiza isanifishe sarufi ya Kiswahili (Whiteley, 1974; Kiango; 2002, Mbaabu, 2007, Hans; 2014).

Japo Maganga (1991) anabainisha kwamba ni vigumu kutoa maana ya Kiswahili sanifu hasa ukizingatia kuwa wengi wamekuwa

[3] Kamati ya Kiswahili iliyoundwa na wakoloni ilibadilishwa jina na kuwa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili na kuwekwa chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baadaye zaidi ikabadilishwa jina na kuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), na mwaka2009 TUKI ikaunganishwa na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuunda TATAKI, yaani Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

wakijiuliza kama hiyo ni lughainayokaribiana na Kiungujaau ni lahaja ndogo ya Kiunguja au ni Kiunguja kilichoharibiwa n.k., anahitimisha kwamba Kiswahili sanifu kinachukuliwa kama lugha rasmi itumikayo katika kazi za chama na serikali, masuala ya uchapishaji wa maandiko ya kitaaluma, na kwenye vyombo vya habari. Hitimisho la Maganga kuhusu maana ya Kiswahili sanifu ndilo msimamo wa makala hii.

Kwa upande mwingine, Kiingereza ni moja ya lugha ambazo asili yake ni familia ya lugha za Kiindo-Ulaya.Hata hivyo, lugha ya Kiingereza imetokana na mwingilianao wa lugha nyingi kama vile Kijerumani kinachosadikika kuchangia 26% ya msamiati, Kifaransa kwa 29%, Kilatini kwa 29%, Kigiriki kwa 6% na lugha nyingine zisizofahamika kwa 10%. Lugha ya Kiingereza ina historia ndefu ya mabadiliko ambayo yanajidhihirisha katika vipindi vikuu vitatu vya kihistoria, na hatimaye kuwapo kwa Kiingereza cha aina tatu: Kiingereza cha Zama za Kale (450-1100 BK), Kiingereza chaZama za Kati(1100 - 1500 BK) na Kiingereza cha Kisasa (tangu miaka ya 1500 BK) (Barbara, 1998). Kwa hiyo, lugha ya Kiingereza inayohusishwa katika makala hii ni Kiingereza cha Kisasa hususani Kiingereza chenye asili ya Uingereza.

Kiingereza chenye asili ya Uingereza ni lahaja ambayo inayojulikana kama Kiingereza sanifu. Hii ndiyo lahaja ya Kiingereza inayotumika kama lugha ya kufundishia nchini Tanzania.

Kiswahili na Kiingereza ni lugha zinazotumiwa na wanataaluma wa Kitanzania huku kila lugha ikiwa na nafasi yake. Lugha ya Kiingereza ni lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na vyuo vikuu huku Kiswahili kikifundishwa kama somo katika ngazi hizo za elimu. Katika ngazi ya chuo kikuu hususani idara au taasisi za Kiswahili, maandiko mengi yanayotumika kufundishia au kujadili nadharia na mambo mbalimbali katika lugha ya Kiswahili ni maandiko ya lugha ya Kiingereza. Mathalani, katika vyuo vikuu mbalimbali nchini Tanzania kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dododoma na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania; wanafunzi wanaosoma shahada za umahiri katika Kiswahili na shahada ya uzamivu katika Kiswahili hutumia maandiko mengi ya lugha ya Kiingereza katika kuandaa tasnifu na tazmili zao.

Aidha, hata maandiko machache yaliyopo yanayohusu ukanushi katika lugha ya Kiswahili yameandikwa kwa kugha ya Kiingereza;

maandiko hayo ni Ashton (1944) katika kitabu kiitwacho "Swahili Grammar (Including Intonation", Beaudoin-Lietz (1999) katika tasnifu iitwayo "Formatives of Tense, Aspects Mood and Negation in the Verbal Construction in Standard Swahili", Ngonyani (2001) katika makala ijulikanayo kama "The Morphosyntax of Negation in Swahili" na Contini-Morava (1989) katika kitabu cha "Discourse, Pragmatics and Semantic Categorization: The Case of Negation and Tense-Aspect with Special Reference to Swahili."

Hivyo, ni kawaida kushuhudia uchambuzi wa masuala mbalimbali (ukiwemo ukanushi) katika lugha ya Kiswahili yakiathiriwa na lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, moja ya njia ya kuwafanya wanaisimu wanaomakinikia suala la ukanushi katika Kiswahili wasiathiriwe na uchambuzi wa ukanushi wa lugha ya Kiingereza ni kulinganisha ukanushi katika lugha hizi mbili, jambo linalofanywa na makala hii.

Utafiti huu unatokana na kupitia maandiko mbalimbali yanayohusu ukanushi katika Kiswahili na ukanushi katika lugha ya Kiingereza; kisha kushadidiwa na mifano ya tungo kanushi kutoka data mbalimbali kama zilivyokusanywa na mtafiti.

**Nadharia ya Isimu Msingi**

Makala hii inaongozwa na nadharia ya Isimu Msingi ya Dixon (1997). Msingi wa nadharia hii ni kuongoza ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya lugha kama vile kanuni za miundo na maumbo za lugha husika. Hii ni nadharia iliyochukua mawazo kutoka katika nadharia za kisasa kama nadharia ya SarufiGeuza Maumbo Zalishi na Sarufi ya Kimapokeo.Baadhi ya watu wamekuwa wakiitazama nadharia hii kama nadharia inayofuata misingi ya Sarufi ya Kimapokeo. Utofauti wake mkubwa ni kwamba, nadharia ya Isimu Msingi inafafanua lugha kulingana na sifa mahususi za lugha husika, tofauti na Sarufi ya Kimapokeo iliyokuwa ikitumia msingi wa lugha za Ulaya kuchambua kila lugha. Hivyo, nadharia hii imesaidia kuongoza ufafanuzi wa maumbo na miundo ya ukanushi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa kuwa kazi ya nadharia hii ni kuongoza uchambuzi wa lugha kulingana na lugha jinsi ilivyo; katika makala hii, nadharia hii imetumika kuongoza ulinganishaji wa maumbo na miundo ya ukanushi katika Kiswahili na Kiingereza.

## Utofauti wa Jumla Kati ya Kiswahili na Kiingereza

Kabla ya kufanya ulinganishaji wa ukanushi katika Kiswahili na Kiingereza, ni vema kuangazia kwa ujumla na kwa ufupi maeneo ambayo lugha hizi zinatofautiana. Tazama suala hilo katikaJedwali Namba 1.

**Jedwali Na. 1: Utofauti katika ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza**

| Na | Vipengele vya Kiisimu | Kiswahili | Kiingereza |
|---|---|---|---|
| 1 | Idadi za fonimu | • 37– Ashton (1951)<br>• 38– Whiteley (1956)<br>• 36–Polome (1967), Nchimbi (1995)<br>• 29 – Mgullu (1999)<br>• 30 – Habwe na Karanja (2004), Kihore, Massamba na Msanjila (2009), Obuchi na Mukhwana (2010), Akidah (2013)<br>• 31– TATAKI (2013) | 44 |
| 2 | Aina ya lugha kimofolojia | Kwa kiasi kikubwa ni lugha ambishi | Kwa kiasi kikubwa ni lugha tenganishi |
| 3 | Asili ya lugha | Lugha za Kibantu | Lugha za Ulaya |

**Chanzo:** Data za Maktabani (2020)

Kama ambavyo inaonekana katika Jedwali Namba 1, kuna tofauti kubwa za jumla kati ya lugha hizi mbili. Aidha, inaonekana kwamba katika lugha ya Kiswahili, wataalamu wana mitazamo mbalimbali kuhusu jambo moja wakati katika Kiingereza, jambo hilo halina mgogoro baina ya wanaisimu; mfano, idadi ya fonimu. Maumbo ya ukanushi katika lugha hizi mbili yanatofautiana kwa namna fulani na yanafanana kwa namna nyingine. Sehemu zinazofuata zimefafanua maumbo ya ukanushi katika lugha hizi mbili.

## Maumbo ya Ukanushi katika Lugha ya Kiingereza

Ukanushi katika lugha ya Kiingereza umejadiliwa na wanaismu mbalimbali kama vile Jespersen (1917), Klima (1964), Dahl (1979), Tottie (1991), Horn and Kato (2000), Horn (2001) na Miestamo (2007).

Jespersen (1917) anaugawa ukanushi katika makundi mawili, ukanushi maalumu na ukanushi usio maalumu. Ukanushi maalumu ni ukanushi unaohusishavikanushi*not* au *no*kujitokeza peke yake vikiwa huru katika tungo, mfano:

a) She is *not*reading a book. 'Hasomi kitabu'
b) They have *no* another option. 'Hawana namna nyingine.'

Aina nyingine ni ukanushi usio maalumu. Huu ni ukanushi unaohusisha vikanushi ambavyo vinaambikwa katika maneno, havijitokezi vikiwa huru kama ilivyo katika ukanushi maalumu. Mifano:

*a)* *Un*kind decision. 'Uamuzi wa kikatili'
*b)* *Il*legal property. 'Mali haramu'
c) Use*less*deal. 'Mpango usio na faida'
*d)* She did*n't*go to school'Hakwenda shule'

Aidha, Tottie (1991) anabainisha aina mbili za ukanushi katika Kiingereza: Ukanushi ambishi na ukanushi huru. Ukanushi ambishi ni ukanushi unaotumia mofimu ambishi za ukanushi kama vile *un-, dis-*,na *–im*. Kwa mfano:

a) Happy –*un*happy.
b) Like- *dis*like.
c) Possible –*im*possible.

Ukanushi huru ni ule unaowakilishwa na maumbo huru ya ukanushi kama vile *not* na *no.* Kwa mfano:

*a)* I do *not* have children. 'Sina watoto'
*b)* I have*no* children. 'Sina watoto'

Zaidi ya maumbo ya ukanushi, Tottie (1991) anatambua kuwapo kwa viambata vya ukanushi[4] katika lugha ya Kiingereza japo yeye hajatumia jina la viambata vya ukanushi kama wataalamu wengine. Yeye kaviita vipashio hivyo kama vishiriki vya ukanushi[5]. Viambata vya ukanushi ni maneno yanayoendana na sentensi au vishazi vilivyopo katika hali ya ukanushi. Mfano wa viambata vya ukanushi kama aelezavyo Heusinger na wenzake (2011) ni *any* na *at all,* mfano:

a) John didn't see *any* people. 'Joni hakuwaona watu wowote.'
b) This isn't white *at all*. 'Hii kamwe si nyeupe'.

---

[4] Hii ni tafsiri ya "negative polarity items"
[5] Hii ni tafsiri ya "incorporating elements"

Aidha, Klima (1964) amekusanya mifano ya sentensi katika lugha ya Kiingereza inayoonesha mitazamo ya wataalamu mbalimbali kuhusu maumbo gani wanayaona ni ukanushi. Jedwali Namba 2 linaonesha sentensi zenye maumbo mbalimbali ya ukanushi na jinsi wataalamu husika walivyojenga utetezi wa kuyatazama kama ni ukanushi.

**Jedwali Na. 2:Maumbo ya Ukanushi na Utetezi wake katika Kiingereza**

| Na. | Sentensi yenye umbo la ukanushi | Utetezi wa mtaalamu |
|---|---|---|
| 1 | *The students did* ***not*** *believe that it had happened*<br>'Wanafunzi hawakuamini kwamba jambo lile lilikuwa limetokea' | Ni umbo lililokubaliwa na wengi |
| 2 | *The students* ***never*** *believed that it had happened.*<br>'Wanafunzi kamwe hawakuamini lilikuwa limetokea' | Ni umbo lililokubaliwa na wengi |
| 3 | *The students* ***hardly*** *believed that it had happened*<br>'Wanafunzi walipata taabu kuamini kwamba lilikuwa limetokea' | Umbo hilo pamoja na *never* yanachukuliwa kama vielezi vya ukanushi |
| 4 | ***None*** *of the students believed that it had happened*<br>'Hakuna hata mmoja aliyeamini kwamba lilikuwa limetokea' | Curme (1931) anasema kwamba *none* ni ukanushi wa *one* |
| 5 | ***Few*** *studentsbelieved that it had happened.*<br>'Wanafunzi wachache waliamini kwamba lilikuwa limetokea' | Poutsma (1929) analiona umbo hilo ni kikanushi dhahiri. Pia, Jespersen (1924) anaona umbo hilo katika miktadha mingi linaonekana ni ukanushi zaidi kuliko uyakinishi |
| 6 | *The students* ***doubted*** *that it had happened* | Jespersen (1917) analiita umbo hilo kama kikanushi cha kitenzi |

| | | |
|---|---|---|
| | 'Wanafunzi walikuwa na mashaka kwamba lilikuwa limetokea' | |
| 7 | *Students were **too** intelligent to believe that it had happened* 'Wanafunzi walikuwa na akili nyingi kiasi cha kuwawia vigumu kuamini kwamba lilikuwa limetokea' | Jespersen (1917) anadai ukanushi pia unaweza kuwakilishwa na umbo hilo huku akitoa mfano wa sentensi hii: She is *too* poor to give us anything; she cannot. 'Yeye ni maskini kiasi kwamba hawezi kutupatia chochote. Hawezi.' |
| 8 | *Students were **unable** to believe that it had happened* 'Wanafunzi hawakuweza kuamini kwamba lilikuwa limetokea.' | Jespersen (1917) analitazama umbo hilo kama moja ya viambishi awali vya ukanushi |

**Chanzo:** Klima (1964)

Klima anahitimisha kuhusu maumbo yaliyoelezwa katika Jedwali Na.2 na utetezi kutoka kwa wataalamu mbalimbali kuwa*not* na *never* ndivyo vikanushi kamili wakati maumbo yanayosalia ni vikanushi visokamili, vikanushi maalumu au vikanushi asilia. Hitimisho la Klima linakaribiana na anachokidai Stockwell na wenzake (1973). Wao waliona kwamba *scarcely*, *seldom*, *rarely* na *barely* ni vikanushi visokamili katika Kiingereza.

Mawazo ya Klima na wengine kuhusu uchambuzi wa maumbo ya ukanushi katika Kiingereza yanaweza kuhitimishwa kwamba lugha hiyo ina vikanushi vya namna mbili. Kundi la kwanza ni vikanushi kamilifu kama vile vikanushi *no*, *not*, *never* pamoja na vikanushi vingine vinavyojitokeza kama viambishi awali au tamati katika maneno kama vile*un, dis* na*less*. Kundi la pili ni vikanushi visokamili kama vile *scarcely*, *seldom*, *rarely*, *few*, *none*, *hardly* na *barely.*

Kwa kuzingatia maelezo ya wanasimu kuhusu ukanushi katika lugha ya Kiingereza, kama ilivyohitimishwa na Klima (1964); kwa ujumla, yako maumbo kamilifu ya ukanushi (vikanushi kamilifu) ambayo yanaweza kuwekwa katika kategoria mbili. Kategoria ya kwanza inajumuisha maumbo yanayojitokeza hasa katika tungosentensi na vishazi. Maumbo hayo ni *no, not/n't* na*never*. Kategoria ya pili ni ile yenye maumbo ya ukanushi yanayojitokeza

kama viambishi awali na tamati katika tungo neno au kirai ambayo ni *il, un, in, less, im, non, mis, ir, de, a,* na *anti*. Ifuatayo ni mifano inayoonesha tungo zenye maumbo ya ukanushi katika kategoria ya kwanza.

a. He is *not* a teacher. 'Yeye siyo mwalimu.'
b. Is this yours? *No*, it is not mine. 'Hii ni yako? Hapana, si yangu.'
c. *Never* will I go there again. 'Kamwe sitaenda huko tena.'
d. You did*n't* (did *not*) come here yesterday. 'Hukuja jana.'

Jedwali Namba 3 linaonesha maumbo kamilifu ya ukanushi katika kategoria ya pili, yale yanayojitokeza hasa katika tungo neno au kirai.

**Jedwali Na. 3: Maumbo ya Ukanushi katika Tungo Neno**

| Umbo la ukanushi | Mfano wake |
|---|---|
| *Il* | *Illegal* 'sio ya kisheria/haramu' |
| *Un* | *Unhappy* 'siyo na furaha' |
| *In* | *Incomplete* 'sio kamili' |
| *Less* | *Useless* 'siofaa' |
| *A* | *Apolitical* 'siopenda siasa' |
| *Non* | *Non-believer* 'asiyeamini' |
| *Anti* | *Anti-corruption* 'siopenda rushwa' |
| *Ir* | *Irresponsible* 'siowajibika' |
| *De* | *Decolonise* 'ondoa ukoloni' |

**Chanzo:** Data za Maktabani (2020)

**Maumbo ya Ukanushi katika Lugha ya Kiswahili**

Kuna wataalamu wengi walioandika kuhusu lugha ya Kiswahili; kwa mfano, Broomfield (1935), Ashton (1944), Polomé (1967), Whiteley (1974), Vitale (1981), Contini-Morava (1989), Schadeberg (1992) na Beaudoin-Lietz (1999). Hata hivyo, wataalamu haowameelezasuala la ukanushi kwa viwango tofautitofauti katika kazi zao. Wataalamu wengi kati ya hao waliotajwa wamejadili suala la ukanushi katika kazi zao kama kipengele tu. Andiko pekee linalojadili ukanushipeke yake ni makala ya Ngonyani (2002).

Maumbo ya ukanushi katika lugha ya Kiswahili yanayotajwa na wataalamu mbalimbali ni yale yanayoambikwa katika maneno hususani vitenzi kama vile *ha (halii), si (si*endi*), ja (*hawa*ja*lima*), ku (*ha*ku*tuelewa*), kuto/to (*ku*to*fika kwake*), sipo/si (*wa*si*potuona*)* na *i (*siib*i).* Pia, yapo maumbo yanayosimama peke yake kama neno linalojitegemea kama vile *hapana* litumikalo kujibu swali la "ndiyo"

au "hapana" na umbo*si* lijitokezalo kama kitenzi kishirikishi kanushi; mfano, *mimi* ***si*** *mwizi.* Ashton (1944) anabainisha kwamba kwa ujumla katika Kiswahili, yako maumbo mawili ya ukanushi: *ha* na *si*, lakini baadaye anaendelea kuyaelezea maumbo hayo pamoja na maumbo mengine kama yalivyooneshwa hapo awali pasi kueleza utofauti wa hadhi ya maumbo hayo. Naye, Beaudoin-Lietz (1999) anatambua kuwapo kwa maumbo matatu tu ya ukanushi ambayo ni *si*, *ha* na *to* huku akieleza kwamba maumbo mengine kama *i, ku* na *ja* siyo maumbo yanayobeba maana ya ukanushi bali hupata dhana ya ukanushi kwa kuhusishwa na vikanushi *si* na *ha.*

Licha ya ukanushi kuelezwa na wataalamu hawa, bado kuna sintofahamu za baadhi ya masuala ya ukanushi katika Kiswahili sanifu zinazohitaji kupatiwa majibu. Sintofahamu ya kwanza ni mgogoro wa *sipo/si,* Ashton (1944) anaeleza kwamba umbo *sipo* linajengwa na viambishi viwili (*si* na *po*) vyenye kazi tofauti ambapo *si* inaonesha ukanushi na *po* inaonesha muda na mahali. Ashton anadai kwamba *sipo* katika kitenzi *asipofika* linamaanisha *wakati ambapo hakijafanyika kitu "when not*", lakini, cha kushangaza, umbo hilo halitenganishwiliwapo ndani ya tungo kuonesha dhima hizo mbili, njeo na ukanushi. Hii ina maana kwamba umbo *sipo* linachukuliwa kama kipashio kimoja kisichotenganishwa. Kwa upande mwingine, Kapinga (1983) anadai *sipo* ni kiambishi cha ukanushi kinachokanusha kiambishi cha masharti *ki-* wakati Wesana-Chomi (2013) anapinga dai hilo kwa hoja kwamba *sipo* ni muundo wa mofimu mbili ambapo mofimu *si* ni ya ukanushi na *po* ni ya masharti.

Aidha, utata mwingine kuhusu lipi linafaa kuwa umbo la ukanushi kati ya *kuto* na *to* linadhihirishwa na mgongano wa mawazo baina ya makundi ya wanaisimu ambapo Ashton (1944) na Ngonyani (2001) wanaamini katika kipashio *kuto*; na Wesana-Chomi (2013) anaamini katika *to*.

Ni jukumu la makala hii kutoa msimamo na mapendekezo ya utatuzi wa mgogoro huo (*kuto/to* na *si/sipo*). Tukianza na suala la umbo lipi linafaa kuwa umbo la ukanuhsi kati ya*kuto* na *to*; kimantiki, linalofaa kuwa umbo la ukanushi ni *to.* Tukizingatia misingi ya Nadharia Isimu Msingi hususani upatanisho wa kisarufi katika sentensi za Kiswahili, sentensi kama vile "kutoiba kwake kunanishangaza"; kipashio cha kwanza *ku* katika neno la kwanza "kutoiba" kinaoana kisarufi na kipashio *ku* kilichopo katika neno la mwisho "kunanishangaza". Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba kama

kipashio *ku* kina dhima yake ya kuoanisha upatanisho wa kisarufi. Pia, *ku* katika "kutoiba" ni kiambishi kisicho ukomo, na *to* inabakia kuonesha ukanushi. Wakati *-ib-* ni mzizi wa neno na *a* ni kiambishi tamati ishilizi.

Aidha, ni nadra sana vipashio (viambishi awali au tamati) katika Kiswahili sanifu kuundwa na silabi mbili. Yaani, neno *kuto* ambalo lina silabi mbili *ku$to* ni nadra kuona linawakilisha kiambishi kimoja katika lugha ya Kiswahili.

Tukimalizia na mgogoro wa *si/sipo*; msimamo wa makala hii ni kwamba umbo la ukanushi hapo ni *si.* Tukifafanua kwa msingi wa Nadharia Isimu Misingi tunabaini kwamba kipashio *po* hufanya kazi yake nyingine kabisa ya kuonesha masharti, ni kosa kukiunganisha kipashio hicho na kipashio *si* na kudai kufanya kazi ya ukanushi. Mfano, *ni-si-po-fik-a* huelezwa dhima za mofimu zinazoundwa nazo kama ifuatavyo:

Ni – kiambishi awali kinachoonesha nafsi ya kwanza umoja
si – kiambishi awali cha ukanushi
po –kiambishi awali cha masharti
fik –mzizi wa neno
a –kiambishi tamati ishilizi

Vilevile, ni nadra sana vipashio (viambishi awali au tamati) katika Kiswahili sanifu kuundwa na silabi mbili. Neno *sipo* lina silabi mbili, hivyo ni vigumu neno hilo kuwa kipashio kimoja.

Aidha, makala hii inayagawa maumbo ya ukanushi yaliyowasilishwa katika aina mbili. Aina ya kwanza ni maumbo ya msingi ya ukanushi na aina ya pili ni maumbo tegemezi ya ukanushi. Maumbo ya msingi ya ukanushi nimuambo ya ukanushi ambayo hudhihirisha mantiki ya ukanushi bayana. Aidha, maumbo hayo hayategemei maumbo mengine ili kukamilisha dhana ya ukanushi. Maumbo hayo ndiyo huonesha msingi wa ukanushi katika lugha ya Kiswahili kwa sababu yanajitokeza bayana zaidi kuliko aina ya maumbo tegemezi ya ukanushi yanayojadiliwa katika aina ya pili. Maumbo ya msingi ya ukanushi ni *si*$_1$, *si*$_2$,*ha, to* na *hapana*kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo ya tungo:

a) Mimi *si*$_1$talima shamba.
b) Wewe *si*$_2$ mkorofi.
c) Wao *ha*watakwenda shuleni.

d) Ku*to*lia kwake kunashangaza wengi.
e) *Hapana*, sijakuelewa.

Maumbo yaliyo katika hati ya italiki ndiyo yanawakilisha maumbo ya msingi ya ukanushi kwa sababu yanarejelea dhana ya ukanushi moja kwa moja.

Aina ya pili ni maumbo tegemezi ya ukanushi. Haya ni maumbo ya ukanushi ambapo ukamilifu wa dhana ya ukanushi hutegemea uwepo wa baadhi ya maumbo ya msingi ya ukanushi. Yaani, kujitokeza kwake kunatokana na kuwapo kwamaumbo ya msingi ya ukanushi ambayo ni *ha* na *si.* Maumbo tegemezi ya ukanushi ni *ku, ta, ja*, *ta* na *i* kama yanavyojitokeza katika mifano ya tungo zifuatazo:
a) Mimi siimb*i.*
b) Yeye ha*ku*lima.
c) Mwalimu ha*ja*fundisha vizuri.
d) Juma ha*ta*imba wimbo leo.

Maumbo ya ukanushi yaliyo katika italiki ndiyo maumbo tegemezi ya ukanushi kwa sababu ni maumbo ambayo hayaoneshi dhana ya ukanushi moja kwa moja bali ukamilishaji wake wa dhana ya ukanushi hutegemea uwepo wa maumbo ya msingi ya ukanushi, *ha* na *si.*

Ijapokuwa katika lugha yaKiswahili hakuna mwanaisimu aliyebainisha viambata vya ukanushi, makala hii imebaini kuwepo kwa dhana hiyo. Mfano wa viambata vya ukanushi kulingana na makala hii ni *ng'o* na *kamwe* kama inavyoonekana katika tungo zifuatazo:

*a)* Siji kwako *ng'oo*
b) Alisema hakanyagi hapa *kamwe.*

Maneno *ng'oo* na *kamwe* yanaonekana kuambatana vilivyo na ukanushi katika tungo zilizotolewa. Maneno hayo yana dhima za vielezi katika tungo hizo.

## Kutofautiana na Kufanana kwa Maumbo ya Ukanushi katika Kiswahili naKiingereza

Baada ya mjadala wa maumbo ya ukanushi katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza, sehemu hii inaonesha mfanano na utofauti wa maumbo ya ukanushi katika lugha tajwa katika misingi

mbalimbali. Vipengele vinavyofuata vimewasilisha kwa ufupi tofauti na mfanano baina ya lugha hizo.

**Tofauti za Maumbo ya Ukanushi kati ya Kiswahili na Kiingereza**

Kwa kiasi kikubwa, maumbo ya ukanushi kati ya lugha hizo yanatofautiana sana. Tofauti hizo zimeonekana katika kategoria mbalimbali: kimaumbo, kimuundo, kiidadi, kiaina, na kinafasi kama inavyoonekana katika JedwaliNamba4.

**Jedwali Na. 4: Tofauti ya Muundo wa Ukanushi kati ya Kiswahili na Kiingereza**

| Kategoria ya Tofauti | Ukanushi katika Kiswahili | Ukanushi katika Kiingereza |
|---|---|---|
| Maumbo ya ukanushi | *si1,si2, ha, ku, ja, i, ta, to*na *hapana* | *not (n't), never, no, il, un, in, less, im, non, mis, ir, de, a,* na*anti* |
| Idadi ya maumbo ya ukanushi | 9 | 14 |
| Aina za maumbo ya ukanushi | Aina mbili:<br>• Maumbo ya msingi ya ukanushi (*ha, si1, si2, to*na *hapana*).<br>• Maumbo tegemezi ya ukanushi (*ku, ta, ja*na *i).* | • Ukanushi wa msingi -maumbo ya ukanushi wa kisintaksia (*not/n't, never* na *no*) yanayojitokeza katika tungo sentensi au kishazi.<br>• Ukanushi wa kiwango cha chini - maumbo ya ukanushi wa kimofolojia (*il, un, in, less, im, non, mis, ir, de, a,* na *anti.*) yanayojitokeza katika tungo neno au kirai. |

| | | |
|---|---|---|
| Nafasi inayokaliwa na umbo la ukanushi katika tungo | • Maumbo mengi ya ukanushi hujitokeza kama kiambishi awali katika kitenzi (*ha*taimba, ***si***taimba), kama kiambishi cha pili cha kitenzi (ha*ja*lima, ha*ku*lima) na kama kiambishi tamati (siend***i***).<br>• Maumbo machache hujitokeza kama vipashio huru (*hapana, si2*) ambayo huweza kujitokeza mwanzoni (*hapana*, sikutaki), katikati (mimi *si* mwalimu) au mwishoni mwa tungo (wewe ni Nabii? *Hapana ).* | • Umbo *not* hujitokeza baada ya kitenzi (he is*not*fair, they are *not* crying). Pia, inaweza kujitokeza mwanzoni mwa tungo (*not* everyone can understand you)<br>• Umbo *no*hujitokeza peke yake kabla ya kiima katika tungo (n*o*, I don't want you here).<br>• Maumbo ya ukanushi katika maneno na virai hujitokeza kama viambishi awali au viambishi tamati (*illegal,useless).* |

**Chanzo:** Uchambuzi wa Mtafiti(2020)

## 4.2 Mfanano wa Maumbo ya Ukanushi Kati ya Kiswahili na Kiingereza

Licha ya maumbo ya ukanushi ya lugha tajwa kuwa na tofauti kama ilivyoelezwa katika kipengele cha 5.0, bado yako maeneo machache ambayo yanaweza kujengewa hoja za mfanano wa maumbo ya ukanushi baina ya lugha hizo. Mosi, katika baadhi ya vitenzi vya lugha zote mbili, kuna viambishivya ukanushi ambavyo hujitokeza ndani ya vitenzi hivyo kama ionekanavyo katika JedwaliNamba5.

**JedwaliNa. 5: Maumbo ya Ukanushi Ambayo ni Mofimu Ambishi katika Kiswahili na Kiingereza**

| Kiswahili | Kiingereza |
|---|---|
| *Si*andik*i* | *I can't write* |
| *Ha*waelew*i* | They do*n't* understand |
| Anatakiwa a*si*elewe | He mus*n't* understand |
| *Ha*tafika leo | He wo*n't* come today |

**Chanzo:** Data za Maktabani (2020)

Katika JedwaliNamba5, maumbo yote ya ukanushi yanaonekana kuwa mofimu ambishi ambazo zimechopekwa katika vitenzi zikiwa zimeambatana na mofimu nyingine. Ifahamike kwamba kwa upande wa Kiingereza suala hilo si la lazima kwa sababu umbo hilo la ukanushi linaloonekana ni mofimu tegemezi (*n't*) linaweza kusimama peke yake kama mofimu huru (*not*) inayofanya kazi ya ukanushi kama ambavyo imekwishaelezwa hapo awali. Kwa mfano:

a) He did*n't* come yesterday
b) He did *not* come yesterday

Mfanano mwingine ni lugha zote mbili kuwa na umbo moja la ukanushi ambalo ni jibu la *hapana* la swali la NDIYO au HAPANA. Katika lugha hizo mbili umbo hilo la ukanushi lina hadhi sawa ya mofimu ambapo lugha zote mbili zinawakilishwa na neno moja ambalo ni mofimu huru. Kiswahili kina neno HAPANA na Kiingereza kina NO.

## Hitimisho

Kwa ujumla, maumbo ya ukanushi katika lugha za Kiingereza na Kiswahili hutofautiana kwa kiasi kikubwa kuliko jinsi yanavyofanana. Kuna sababu mbalimbali za msingi za kuwapo kwa tofauti hizo. Mosi, lugha hizo zina asili tofauti ambapo Kiswahili asili yake ni Kibantu wakati Kiingereza asili yake ni lugha za Kiindo-Ulaya. Pia, Kiingereza ni lugha iliyotokana na mwingiliano wa lugha nyingi kama Kilatini, Kijerumani, Kifaransa na Kigiriki, tofauti na Kiswahili ambacho mwingiliano wake na lugha nyingine si mkubwa ukilinganisha na Kiingereza.Aidha, kwa kiasi kikubwa, Kiswahili ni lugha ambishi ambapo maneno yake mengi hujengwa kwa mfuatano wa viambishi wakati lugha ya Kiingereza kwa kiasi kikubwa ni lugha tenganishi ambapo tungo zake hujengwa na mofimu huru. Kwa hivyo, uchambuzi wowote wa ukanushi katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza unapaswa uzingatie hali hiyo ya kufanana kiasi na kutofautiana kwa lugha hizo ili kufanya

uchambuzi ambao hautasababisha lugha moja kuathiri uchambuzi wa ukanushi wa lugha nyingine. Tahadhari hii inapaswa kuzingatiwa sana hasa na wanaisimu watakaojadili ukanushi katika lugha ya Kiswahili ili wasije wakajikuta wanatumia misingi ya uchambuzi wa lugha ya Kiingereza kuchambua ukanushi katika lugha ya Kiswahili kwa sababu hata maandiko ya mwanzo kuhusu sarufi ya Kiswahili yameandikwa kwa Kiingereza. Vilevile, ukanushi katika lugha ya Kiingereza umeelezwa kwa kina sana na wanaisimu wengi ukilinganisha na Kiswahili; na wanasimu wengi wa Kiswahili husoma machapisho ya lugha ya Kiingereza kama marejeleo katika maandiko yao ya Kiswahili.Kutokana na hali hiyo, ni rahisi sana wanaisimu wanaomakinikia lugha ya Kiswahili kuathiriwa na uchambuzi uliofanywa katika lugha ya Kiingereza kuhusu suala linalomakinikiwa kama vile ukanushi na vipengele vingine vya lugha.

Aidha, kwa kuwa makala hii haijaangazia masuala ya unyume na ukanushi uwili katika lugha zinazolinganishwa, inapendekezwa makala au tafiti zijazo zimakinikie masuala hayo.

**Marejeleo**

Akidah, M. A. (2013). Phonological and Semantic Change in Language Borrowing. The Case of Arabic Words Borrowed into Kiswahili. *International Journal of Education and Research*, 1(4), 1-20. Kutoka www.ijern.com/images/April2013/42.pdf

Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar (Including Intonation).* London: Longman Group Ltd.

Barbara, F. (1998). *A History of English: A Sociolinguistic Approach*. Oxford: Blackwell.

Beaudoin-Lietz, C. (1999). *Formatives of Tense, Aspects Mood and Negation intheVerbal Construction in Standard Swahili*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Memorial University of Newfoundland.

Contini-Morava, E. (1989). *Discourse Pragmatics and Semantic Categorization: The Case of Negation and Tense-Aspect with Special Reference to Swahili*. Berlin: Mouton de Gruyter.

Crystal, D. (1993). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. Blackwell: Oxford University Press.

Curme, G. O. (1931). *Syntax*. Boston and Tokyo: D.C. Heat and Company & Maruzen Company Ltd.

Dahl, Ö. (1979). Typology of Sentence Negation.*Linguistics* 17:79–106.

Haegeman, L. (1995). *The Syntax of Negation*. New York: Cambridge University Press.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi*. Nairobi: Phoenix Press.

Jespersen, O. (1917). *Negation in English and other Languages*. Copenhagen: A. F. Host.

Heusinger, K., Portner, P. & Maienborn, C. (2011). *The Handbook of Natural Language Meaning*. Berlin: Mouton de Gruyter.

Horn, L. (2001). *A Natural History of Negation*. Chicago: CSL1 Publications.

Horn, L. & Kato, Y. (2000). *Negation and Polarity: Syntactic and Semantic Perspectives.* Oxford: Oxford University Press.

Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kiango, J. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki. *Swahili Forum,* IX:143-154.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. & Msanjila, Y.P. (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA).* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Klima, E. S. (1964). Negation in English. ni J. A. Fodor & J. J. Katz (eds.). *TheStructure of Language*: *Readings in the Philosophy of Language.* New York: Prentice-Hall: 246-323.

Lindstad, A. M. (2007). Analyses of Negation: Structure and Interpretation. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Oslo.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Maganga, G. (1991). *A Study of the Morphophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi.* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, P. B., Kihore, Y. M. & Hokororo, J. I. (2012). *Sarufi Miundo ya Kiswahili: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Miestamo, M. (2007). Negation: An Overview of Typological Research. *Language and Linguistic Campass,* 5(1): 552–570.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longman.

Nchimbi, A. S. (1995). Je, Mang'ong'o ni Fonimu au si Fonimu katika Kiswahili Sanifu? *Baragumu,* 25-39. Maseno: Chuo Kikuu cha Maseno.

Ngonyani, D. (2001). The Morphosyntax of Negation in Swahili. *Swahili Forum*, VII:17-33.

Obuchi, S. M. & Mukhwana, A. (2010). *Muundo wa Kiswahili. Ngazi na Vipengele*. Nairobi: A~Frame Publishers.

Poutsma, H. (1929). *A Grammar of Late Modern English. Part 11: The Sentence. Second Half.* Groningen: P. Noordhoff.

Polomé, E. (1967). *Swahili Language Handbook.* Washington: Center for Applied Linguistcs.

Schadeberg, T. C. (1984). *A Sketch of Swahili Morphology*. Köln: Rüdiger Köppe Verlag.

TATAKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Toleo la 3. Nairobi: University of Dar es Salaam na Oxford University Press.

Tottie, G. (1991). *Negation in English*. San Diego, Calif: Academic Press. Imepakuliwa 15/01/2016 kutoka https://searchworks.stanford.edu/view/726258

Vitale, A. (1981). *Swahili Syntax.* Dordrecht: Foris Publications.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TATAKI.

Whiteley, W. (1974). *Swahili: The Rise of a National Language*. London: Methuen.

Whiteley, W. H. (1956). *Studies in Swahili Dialect 1: Kimtang'ata*. East African Swahili Committee.